

Dhima ya Fasihi katika Mshikamano wa Kitaifa: Tathmini ya Tungo za Tom Olali

Mwenda Mbatiah

Chuo Kikuu Nairobi, Kenya

Ikisiri

Makala haya yanajadili suala la dhima ya fasihi katika kuleta mshikamano wa kitaifa. Hili ni suala zito barani Afrika, ambapo mchakato wa kujenga uitaifa ulioanza katika harakati za ukombozi, unakabiliwa na changamoto nyingi. Nchini Kenya, kwa mfano, tumeshuhudia matukio kadha ambayo yametishia kuliporomosha taifa lililozaliwa mwaka wa 1963. Mfano mzuri ni vurugu ya baada ya uchaguzi mwaka wa 2007 hadi 2008. Msimamo wetu ni kwamba fasihi ya kitaifa inaweza kutoa mchangano muhimu katika kuleta mshikamano wa kitaifa na amani ya kudumu. Lakini swali ni je, ni fasihi ya aina gani inayoweza kufanikisha hilo? Katika kutafuta jawabu la swali hilo, tunazithmini kazi za Tom Olali, ambaye ni mmojawapo wa waandishi wa Kiswahili nchini Kenya. Kazi zinazohusika ni: *Mafamba* (2008), *Watu wa Gehenna* (2012) na *Mashetani wa Alepo* (2015). Tumetathmini vipengele vya fani na maudhui ya kazi hizo mintarafu ya mada ya iliyotajwa hapo juu.

Maneno Muhimu: Dhima, Fasihi, Mshikamano, Kitaifa.

Utangulizi

Kiwakati, mataifa ya Kiafrika ni machanga yakilinganishwa na yale ya mabara mengine ya dunia kama vile Ulaya, Amerika Kusini na Kaskazini na hata Asia. Historia ya kubuniwa kwayo inaanza katika nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa, ambapo kulingana na Okoth (2006), sehemu kubwa ya bara la Afrika iligawanywa kati ya mataifa makuu ya Ulaya katika mchakato unaorejelewa kama “kinyang’anyiro na mgawanyo wa Afrika”. Kilele chake kilikuwa kongamano la Berlin mwaka wa 1884-5. Uchanga huu wa mataifa ya Kiafrika unachangia hali yake ya sasa ambayo inajadiliwa hapa chini.

Japo kuna tofauti hapa na pale, mataifa ya Kiafrika yana sifa kadha za kijumla. Kwanza, yamebaki nyuma kimaendeleo. Pili, yamo katika awamu ya ukoloni mamboleo ambapo kwa kiwango kikubwa yanayategemea mataifa yaliyoendelea kiuchumi. Tatu, yanakosa uthabiti wa kisiasa, na hivyo kutumbukia

katika machafuko ya mara kwa mara na hata vita vya wenyewe kwa wenyewe. Mifano michache ya hali hii ni kama ifuatayo: (a) Vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Uganda kati ya NRA ikiongozwa na Yoweri Museveni na majeshi ya serikali kati ya mwaka wa 1981 na 1986 (b) Vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Somalia katika miaka ya 1980 ambapo makundi kadha ya wapiganaji yalipambana na serikali ya kijeshi ya Siad Barre. Hatimaye, makundi hayo yalimwangusha mwaka wa 1991, na matokeo yakawa kusambaratika kwa taifa la Somalia. (c) Vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Rwanda kati ya majeshi ya serikali na waasi wa RPF kuanzia mwaka wa 1990, ambavyo vilijumuisha mauaji ya kikabila mwaka wa 1994. (d) Machafuko ya baada ya uchaguzi nchini Kenya mwaka wa 2007-8.

Ukosefu wa uthabiti wa kisiasa na sifa nyingine zilizotajwa hapo juu yana uhusiano na jinsi mataifa ya Kiafrika yalivyobuniwa. Wakoloni waliyabuni mataifa hayo kwa kuunganisha kiholela makabila ya Waafrika ambayo awali yalikuwa jumuiya huru zilizojitawala na kujitegemea. Mara nyingine, makabila yaliyohusika yalikuwa ya mahasimu. Kuyaweka pamoja makabila hayo bila hiari kulizua mivutano kati yao ambayo imeendelea kujitokeza hata baada ya uhuru wa bendera. Hii ndiyo hali inayorejelewa kama ukabila. Hali ya kuwepo kwa jumuia huru ndani ya taifa moja imepelekea baadhi ya wanazuoni kuchukua mwelekeo tofauti kuhusiana na suala la utaifa. Badala ya kuchukulia Kenya kama taifa moja, kwa mfano, wanazuoni kama Ngugi wa Thiong'o wanaichukulia kuwa ungitaifa. Hivi ni kusema kwamba makabila zaidi ya arbabini yanayounda Kenya yana hadhi sawa, na ni mataifa kamili ndani ya taifa kubwa. Changamoto zinazoyakabili mataifa ya Kiafrika zimeshughulikiwa na waandishi wengi wa Kiswahili na wanaoandika kwa lugha za kigeni. Waandishi wanaohusika wameangazia changamoto hizo kwa kushambulia uongozi mbaya kama chanzo cha matatizo mengi yanayowakumba Waafrika. Waandishi wanapoangazia uozo wa kisiasa katika kazi zao, wanachangia kuuzindua umma kuchukua hatua zifaazo. Katika makala haya, tunautathmini mchango wa mwandishi immoja wa Kiswahili katika tungo zake tatu.

Dhima ya Fasihi kwa Taifa na jinsi Fasihi inavyotekeleza Dhima hiyo

Kabla ya kushughulikia tungo za Tom Olali, ni muhimu kwanza kujadili kwa usupi dhima ya fasihi katika taifa lolote, na jinsi fasihi inavyotekeleza dhima hiyo. Wellek na Warren (1949) wanasisitiza kwamba lazima dhima ya fasihi itokane na maumbile yake. Yaani haifai kuitwika fasihi dhima inayopingana na nduni zake za kiujumi na kijamii. Kimsingi, dhima hiyo ni kuburudisha na kuzindua sawia. Hili ni wazo la tangu enzi ya Ugiriki na Urumi ya kale lililozaa wanadharia kama Plato, Aristotle, Horace na wengineo. Akizungumzia sanaa kwa jumla, ambamo fasihi imejumuishwa, Ernst Fischer (1959) anasema kwamba katika asili yake, sanaa ilikuwa mazingaombwe ambayo binadamu alitumia kama nyenzo ya kuuelewa na kuutawala uhalisi. Halafu anaendelea kueleza (uk.14) kwamba

“Dhima hii ya fasihi kama mazingaombwe imeipisha dhima ya kumulika mahusiano ya kijamii, kuzindua watu wanoishi katika jamii buye, kuwasaidia watu kuutambua na kuubadilisha uhalisi wa kijamii.” (TY) Baadaye, anafafanua kwamba pamoja na dhima yake mpya ya kufunza na kuzindua, sanaa hubakisha chembechembe za mazingaombwe. Vazquez (1973:119) anatoa mawazo juu ya dhima ya fasihi ambayo hayatofautiani na yale yaliyotajwa hapo juu, lakini anaongeza sifa muhimu za fasihi kama njia ya mawasiliano inayowashirikisha watu:

Msanii wa kweli ana uwezo wa kubuni media bora ya mawasiliano kuliko lugha ya kawaida. Kitu anachozua sio sanaa kwa ajili ya sanaa, bali nyenzo ya kuwafikia watu. Sanaa ya kweli hufichua vipengele muhimu vya hali ya binadamu kwa njia ambayo inavutia na kuwashirikisha watu. Kwa hivyo sanaa isiyowasiliana inaikana sifa muhimu ya sanaa. (TY)

Suala zito la fasihi kuweza kuwasiliana na hadhira yake ambalo Vasquez analizungumzia hapa litashughulikiwa zaidi baadaye. Mawazo yaliyorejelewa hapo juu yanaelekea kuwiana, licha ya kuwa ni ya wanadharia wa mataifa mbalimbali. Hii ni ithibati ya kwamba katika mtalaa wa fasihi, kuna maelewano juu ya maumbile na dhima ya fasihi bila kujali mipaka ya kitaifa. Hata hivyo, kwa vile tunazungumzia fasihi ya Kiafrika, ya Kiswahili haswa, na katika muktadha wa taifa la Kiafrika, ni muhimu kuukita mjadala unaohusika katika muktadha wa Afrika. Inahalisi kujiuliza fasihi ilikuwa na dhima gani katika jumuiya zetu za kijadi na kuhusisha jawabu na hali yetu ya sasa.

Suala zito la dhima ya fasihi katika jumuiya za kijadi za Kiafrika limeshugulikiwa na vigogo kadha wa fasihi ya Kiafrika. Mmoja wao ni Ngugi wa Thiong'o (1972) ambaye anasema: “Sanaa ya Kiafrika, tunaweza kusema kwa ujumla, ilikuwa imeelekezwa kwenye jumuiya. Na kutohana na sifa yake ya kuwa mali ya umma, utamaduni ulisaidia kuunganisha jamii.” (TY) Mwelekeo huu ni tofauti na ule wa tamaduni za Kimagharibi ambapo huwa kuna mwachano kati ya msanii na ulimwengu wake kwa upande mmoja, na jamii anamoishi kwa upande mwingine. Katika jamii zinazohusika, msanii aghalabu hujitokeza kama mwasi anayeishi pembezoni mwa jamii. Kama maelezo ya hapo juu yanavyoonyesha, hali ya msanii wa Kiafrika ni kama kinyume na hiyo. Hivi ni kwa sababu msanii wa Kiafrika ni mwanajamii. Kazi yake inafungamana na matakwa na matarajio ya jamii. Sanaa yake inalengwa kuifaidi jamii. Faida mojawapo ni kudumisha mshikamano wa kijamii. Kwa vile jamii ya Kiafrika ambayo ndiyo hadhira ya mwandishi wa leo ni taifa, tunaweza kusema kwamba kazi yake huwa na lengo la kudumisha mshikamano wa kitaifa. Je, hili hutokeaje kiutendaji? Hili hutokeea mwandishi anapoandikia matatizo yanayowakabili wanajamii, na ambayo yanahitaji ufumbuzi. Mwandishi anapoandikia juu ya masuala yanayohusiana na ufisadi kama vile wizi wa mali ya umma, hongo, mapendeleo katika ajira na kupandishwa vyeo, ubaguzi katika misingi ya kijinsia na kikabila, ananuia

kuwafanya wanajamii wayaelewe zaidi na wachukue hatua za kupambana nayo. Mwandishi anapoandikia masuala ya kijamii kama hayo, anaishirikisha jamii katika uandishi wake. Aidha, anashiriki katika ujenzi wa taifa lake.

Njia nyingine ambayo mwandishi wa Kiafrika hutumia kudumisha mshikamano wa kitaifa ni kuandikia thamani za kitaifa na kuzitokuza thamani hizo. Tunatumia neno “thamani” kama istilahi inayomaanisha kanuni za maadili na imani juu ya wema na ubaya ambazo huongoza matendo ya watu binafsi au jumuiya. Kwa mfano katika jumuiya za kijadi za Kiafrika, udugu na heshima kwa wazee zilikuwa thamani za kimsingi. Ziliongoza matendo ya watu kwa sababu kila mtu alitarajiwa kutagusana na watu wote kana kwamba walikuwa ndugu zake, kwa kupendana na kusaidiana. Pia alitarajiwa kutambua mamlaka ya wazee na kuwatii. Thamani nyingine muhimu katika mataifa ya Kiafrika, na ambazo wasanii huandikia ni kama vile uzalendo, demokrasia, haki za binadamu, utunzaji wa mazingira na kufuata sheria.

Tumetaja hapo juu kwamba mwandishi wa Kiafrika ni mwanajamii anayezingatia ndoto na maazimio ya jamii yake, ambayo ni taifa zima. Kwa hali hii, hawezi kuwa mwasi anayeishi nje ya jamii, na hivyo aliye huru kujandikia anavyopenda juu ya anachopenda. Hawezi, kwa mfano, kuandika juu ya mahusiano ya kimapenzi wakati ambapo jamii yake imelemewa na makovu ya vita vya wenyewe kwa wenyewe. Hivi ni kusema kuwa uteuzi wa maudhui na dhamira ni wajibu muhimu kwa mwandishi wa Kiafrika. Lazima maudhui na dhamira ya kazi yake yaendane na mahitaji ya jamii yake. Kwa kusema hivi, tunachukulia kwamba hadhira ya mwandishi ni jamii yake. Ni upotovu mtupu kwa mwandishi kutunga kazi kwa kulenga hadhira ya nje huku akipuuza jamii yake. Waandishi wengi wa Kiafrika wamekiri waziwazi kwamba wanaziandikia jamii zao ili kuwazindua wanajamii. Kwa mfano, Euphrase Kezilahabi amewahi kusema katika mahojiano kwamba anawaandikia wakulima ili waweze kuilewa vyema zaidi hali yao (taz. jarida la *Lughha*, juzuu 1, 1977). Ngugi wa Thiong'o, mara nyingi, ameeleza kwamba analiandikia tabaka la wafanyakazi na mafalahi ili kulizindua na kuliwezesha kuchukua hatua za kuleta mapinduzi yatakayouporomosha mfumo wa kibepari. Kwa jumla, masuala ya hadhira na maudhui yanaenda pamoja, kwa kuwa mwandishi anapoilenga hadhira maalum, anateua maudhui yaliyo na manufaa kwa hadhira hiyo.

Kwa mfano, na kufuatana na msimamo wa Kezilahabi uliotajwa hapo juu, riwaya yake kama vile *Gamba la Nyoka* (1979) inashughulikia maudhui ya utekelezaji wa sera za Ujamaa nchini Tanzania chini ya utawala wa Mwalimu Nyerere. Hili lilikuwa badiliko kuu ambalo liliwaathiri walio wengi nchini Tanzania. Kihistoria na kijamii, hili ndilo lililokuwa tukio muhimu zaidi nchini humo katika miaka ya sabini. Umuhimu wa kilimo kama nguzo ya mfumo mpya ni wa kipaumbele. Mwishoni mwa riwaya, babake Maombosasa, mzee Farjalla, ambaye ni mkulima anayetumia vifaa vya kisasa kama trekta, anasawiriwa kama

kiwakilishi cha watu watakaofaulisha Ujamaa. Hapa tunaona wazi kwamba mwandishi ametimiza ahadi yake ya kuwaandikia wakulima. Amewasawiri kama walio na nafasi muhimu katika ujenzi wa jamii mpya katika misingi ya Ujamaa. Uteuzi wa hadhira wa Ngugi na Kezilahabi unafaa kwa sababu unawalenga walio wengi katika taifa, na hivyo kutoa mchango muhimu katika kuleta mshikamano. Fasihi inayolenga hadhira pana ya watu wa kawaida kama wakulima na wafanyakazi ina manufaa makubwa zaidi kwa taifa kuliko ile inayolenga hadhira finyu kama ile ya wanazuoni wa ndani na nje ya taifa.

Ili kufanikisha dhima ya fasihi katika kuleta mshikamano wa kitaifa, sio hadhira na maudhui tu ambayo mwandishi wa Kiafrika anapaswa kuzingatia, bali pia uhalisi wa kwamba kazi yake ni tendo la mawasiliano. Hivi ni kusema kwamba kazi yoyote ya kifasihi inawakilisha mawasiliano ya kimaandishi kati ya mwandishi na hadhira yake. Ili kufanikisha mawasiliano, suala la uteuzi wa lugha na mtindo wa lugha hiyo ni muhimu. Tunazungumzia uteuzi wa lugha kwa sababu hali ya matumizi ya lugha katika mataifa ya Kiafrika baada ya uhuru wa bendera ni wa ungilugha. Kuna lugha nyingi za Kiafrika, na pia lugha ya kikoloni ambayo, kutokana na mataifa ya Kiafrika kudhibitiwa na ukoloni mamboleo, ndiyo inayotumiwa katika shughuli zote muhimu za kitaifa. Hata pale ambapo lugha ya Kiafrika kama Kiswahili inatambuliwa kisheria kama lugha rasmi – kama ilivyo nchini Kenya – bado lugha ya kikoloni inapendelewa.

Ni katika mazingira haya ambapo tangu 1960, umevuma mjadala mkali juu ya lugha ya kuandikia fasihi ya Kiafrika. Mjadala huo umeshughulikiwa na Nazareth (1978) Chinweizu na wengine (1983), Ngugi wa Thiong'o (1981), na wengineo. Msimamo wa vigogo hao ni kwamba fasihi ya Kiafrika inafaa kuandikwa kwa lugha ya Kiafrika. Tunaunga mkono msimamo huo. Akizungumza juu ya umuhimu wa mtu mweusi kuwa na lugha yake ambayo sio mali ya mkoloni, Frantz Fanon (1967) anasema: "Mtu ambaye anamiliki lugha, humiliki ulimwengu unaowakilishwa na kuwasilishwa na lugha hiyo". Naye Ngugi analihuisha suala la lugha ya fasihi ya Kiafrika na ubeberu, ambao awamu zake za ukoloni na ukoloni mamboleo zinaendelea kudhibiti sio tu uchumi, bali pia siasa na tamaduni za Kiafrika. Kukataa kutumia lugha hizo na badala yake kutumia lugha za Kiafrika ni hatua muhimu katika kujikomboa.

Katika Afrika Mashariki, na hasa nchini Kenya, suala la uteuzi wa lugha ya kuandikia sio tatizo kubwa kwa sababu tuna Kiswahili, ambacho ndicho lugha ya walio wengi. Hii ndiyo lugha ambayo inatumiwa na watu wa kawaida, hasa matabaka ya wakulima na wafanyakazi, katika shughuli zao za kila siku. Kufuatana na maoni ya Ngugi yaliyotolewa hapo juu, uamuzi wa kutumia lugha kama hii katika uandishi ni wa kiuzalendo. Uamuzi huo ni hatua ya kuchangia katika kulikomboa taifa kutokana na ukoloni mamboleo. Jambo hili lina uhusiano wa moja kwa moja na mshikamano wa kitaifa. Hivi ni kwa sababu taifa ambalo halidhibitiwi na wenyeji, na badala yake linatumiwa na wageni kwa maslahi yao,

ni vigumu kuweza kuwa na mshikamano. Historia ya utawala wa kikoloni inaonyesha kwamba mkakati mmoja ambao wakoloni walitumia kuwadhibiti watawaliwa ni kuwagawanya.

Je, suala la fani (inayojumuisha mtindo) linahusianaje na azma ya kuwa na fasihi ya kitaifa ambayo inakidhi mahitaji ya kitaifa kama vile kuleta mshikamano? Fani ni jumla ya mikakati na mbinu za kisanaa ambazo zinatumiwa kuwasilisha maudhui. Hapo juu, tumegusia suala la maudhui yafaayo kwa hadhira ifaayo. Mbali na kuteua lugha inayotumiwa na walio wengi, mwandishi wa Kiafrika anawajibika kutumia fani ambayo itasahilisha mawasiliano kati yake na hadhira. Kazi ya kifasihi kuwa na fani ifaayo sio jambo linalotokea kisadfa, bali linatokana na uamuzi wa mwandishi. Anaweza kutumia mtindo sahili ambao utaiwezesha hadhira yake ya walio wengi kuilewa kazi yake, au anaweza kutumia mtindo mgumu ambao unaweza tu kueleweka na hadhira ndogo kama ile ya wasomi. Waandishi wasioandikia hadhira ya walio wengi, aghalabu huwa na mtazamo usio wa kimaendeleo na usio wa manufaa kwa taifa. Akizungumzia waandishi kama hao, Chinweizu (na wenzake) anawaita wafuasi wa ukoloni na ukoloni mamboleo, ambao hujitahidi kutumikia hadhira na washauri wao wa Ulaya na Marekani kwa kuiga mitindo ya usasa. Anasema kuhusu maandishi yao: “Usahili wa msamiati unashushwa thamani, msamiati mgumu unatukuzwa, dhamira za Kiafrika ambazo zingefaa katika muktadha wa Kiafrika zinapuuzwa” (uk. 241). Tutayahuisha mawazo haya na tungo za Tom Olali ambazo zinashughulikiwa katika sehemu inayofuata.

Mchango wa Tungo za Tom Olali

Tom Olali ni mmoja wa waandishi wa kizazi kipyä katika Kiswahili nchini Kenya. Kitaaluma, amefuata mkondo wa waandishi wengine wa kizazi hicho, ambao ni wanazuoni waliobobea taaluma za Kiswahili. Ana shahada ya kwanza, uzamili na uzamivu katika masomo yanayohusiana na Kiswahili. Kwa sasa ni mhadhiri mwandamizi wa fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi. Uandishi wake ulianzia 2008 ambapo kazi yake ya kwanza: *Mafamba*, ilichapishwa. Ilifuatwa kwa karibu na *Watu wa Gehenna* (2012) na *Mashetani wa Alepo* (2015). Kazi zote tatu zinawiana kwa njia nyingi, kama maelezo ya hapa chini yatakavyobainisha.

Katika kuzitathmini kazi hizo na kuzihusisha na suala la mchango wake katika kuleta mshikamano wa kitaifa, inahalisi kuzungumzia, kwa ufupi, uainishaji wake. Hivi ni kwa sababu uainishaji unahusiana na fani na maudhui yake. Aidha, uainishaji wa kazi za kifasihi ni hatua muhimu katika kuzifasiri. Mpaka hapa, tumejiepusha kimakusudi na kuzirejelea tungo zinazohusika kama “riwaya”. Hivi ni kwa sababu, riwaya, kama utanzu unaojengeka kutoptana na simulizi ndefu ya kinathari iliyokitwa katika mandhari maalum ya kiwakati na kijamii, ina nduni ambazo zinaipambanua na tanzu nyingine. Chambilecho

Mlacha na Madumulla (1991:1), “Riwaya ni hadithi iliyotungwa ambayo ina urefu wa kutosha, visa vinavyooana na ambayo inazingatia suala la muda.” Kwa ufupi, nduni kuu za riwaya ni kama zifauatazo:

- a) Taswira ya mandhari ya kiwakati, kijiografia na kijamii ambayo yanaweza kuhusishwa na matukio halisi katika muktadha halisi wa kijamii.
- b) Kiwango cha uhalisia ambacho ni cha juu kuliko ramsia – kwa kutambua kwamba riwaya inaweza kuchanganya fantasia na uhalisia, na ndiposa tunapata uhalisiajabu.
- c) Wahusika ambaao, kwa kiasi kikubwa, wana sifa za wanadamu halisi, na ambapo angalau baadhi yao wamekuzwa vya kutosha.
- d) Urefu wa kutosha ambaao unaiwezesha riwaya kuwa changamano katika ukuzaji wa wahusika na usawiri wa mandhari ya kiwakati, kijiografia na kijamii.
- e) Simulizi ndefu ambayo ina msuko unaotokana na mfululizo wa visa vinavyohusiana.
- f) Zao la ubunifu wa mwandishi ambalo ni tofauti na wasifu na maelezo ya kihistoria yanayorejelea watu na matukio ya ukweli.

Sio lazima riwaya zote ziwe na nduni hizo zote kwa kiwango sawa, na ni muhimu kusisitiza kwamba huu ni utanzu ulio na unyumbufo mkubwa. Aidha, kuna aina mbalimbali za riwaya. Uainishaji hutegemea mambo kama vile muundo, ndiposa tuna riwaya ya kibarua, riwaya teti, n.k. Pia kuna uainishaji unaotegemea mandhari ya kiwakati na kijiografia, ndiposa tuna riwaya ya kihistoria, riwaya ya kimji, riwaya ya shamba, n.k. Hivi vyote ni vitanzu vya riwaya.

Ni wazi kwamba kazi tatu za Olali zinakiuka, kimakusudi, nduni za riwaya zilitotajwa hapo juu, na kwa hivyo haifai kuziainisha chini ya utanzu unaohusika. Kabla ya kutoa ithibati, ni muhimu kusisitiza kwamba kusema kazi fulani sio riwaya ni tofauti na kusema kwamba ni kazi duni. Tunaposema sio riwaya, tunamaanisha kwamba ni kazi ambayo kiutanzu, ni tofauti na riwaya, na tunawajibika kufikiria jinsi ya kuiainisha.

Tukirejelea kazi za Olali, tunaona kwamba kwanza, nduni ya uhusika katika utanzu wa riwaya inakiukwa. Hivi ni kwa sababu wahusika wa kazi hizo wana sifa ambazo ni tofauti sana na binadamu halisi, na wala hawakuzwi. Sura, majina, maumbo na sifa zao nyingine ni za kiajabuajabu. Kwa kweli wanalingana zaidi na mazimwi au majini kuliko binadamu halisi. Katika *Mafamba*, kwa mfano, wahusika tunaokutana nao mwanzoni ni Arijojo na Maotad. Tunaambiwa juu ya Arijojo kwamba rangi yake inabadilikabadilika kati ya kijani kibichi na kijivu kutegemea aliko wakati wowote: ikiwa yumo ndani au nje ya kibanda chake.

Kuhusu umbo lake, tunaambiwa kwamba alikuwa “sawa na kidurango”; aidha “Nywele zake zilisokotana zikaunga mfano wa neno YATSRA.” (uk. 2) Naye Maotad, mbali na maajabu mengine, ana umri wa miaka 720 (uk. 3). Kuna mhusika mwingine anayeitwa Amrao, ambaye “Urefu wake ulikuwa futi 20 na mwenye uso wa kuvnjari.” (uk.24) Katika *Watu wa Gehenna*, tunaelezwa jinsi mwalimu Baya alishtuka alipoyagundua maumbile ya Mishi, ambaye alimchukulia kuwa kisura: “Alitazama miguu yake aione alivaa viatu gani vyenye kutoa mliongungedhani mbao ikigonga sakafu. Moyo ulimpasuka kwani hakuyaamini macho yake. Mishi hakuwa amevaa viatu vya mchuchumio bali miguu yake ilikuwa ya kwato za ng’ombe.” (uk. 110) Pia kuna viumbe ambao ni nusu wanyama na nusu binadamu. Kwa mfano katika *Mashetani wa Alepo*, tunaambiwa juu ya samaki anayesimulia hadithi ya maisha yake: “Samaki yule alianza kusema kisa chake. Alianza kusimulia. Ni vigumu kujuwa ikiwa alikuwa samaki ama binadamu. Alivyosimulia kisa chake, alikuwa ni kama binadamu. Pia kama samaki.” (uk. 14)

Maumbile na tabia za viumbe wanaopatikana katika tungo za Olali, na ambao wanachukua nafasi ya wahusika katika utanzu wa riwaya, ni sehemu ya fantasia ya tungo hizo. Fantasia hiyo, japo ina uhalisia hapa na pale, inachangia pakubwa kuzinyima kazi hizo sifa ya riwaya, mintarafu ya uhusika. Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa mwandishi amesawiri, kimakusudi, viumbe wa ajabu ili kuvunja kaida mojawapo ya riwaya, ambayo ni kutumia binadamu wa kawaida kama wahusika. Uvunjaji huu wa kaida za riwaya hauhusiani na uhusika tu, bali pia mandhari. Katika tungo zinazohusika, mandhari tunayochorewa ni ya kiajabuajabu, na yasiyoweza kuhushishwa na mahali au jamii yoyote maalum. Hivi ndivyo mandhari ya Gehenna, sehemu ya nchi iitwayo Kiafra, yanavyoelezwa:

Yapo matanuu manne yenyе moto mkali wa kutesea watu milele.... Zipo volkano nne zilizo na vilele juu na chini na zenyе bonde linalopasua kati-kati. Volkano hizo zinaelea katika ombwe isiyopenyeka. Volkano hizi ni kubwa, zinatengana kwa maelfu ya maili, kandokando, chini na juu. Ombwe hiyo inanyosha hadi mahali wazi pasipo mwisho....Kuna lava Inayobubujika kila mahali. (uk.1)

Jina la mahali panapohusika limetumiwa kuwakilisha Jahanamu. Katika imani za kidini, jahanamu ni mahali ambapo watu waliomiasi Mungu watapelekwa ili kuadhibiwa milele. Nalo jina “Kiafra” linatokana na matumizi ya mbinu ya anagramu, ambapo mpangilio wa herufi za jina “Afrika” umepinduliwa. Hili limefanya ili msomaji aweze kuyahusisha maovu yanayobainishwa na kazi zinazohusika na bara la Afrika. Hata hivyo, fasiri yetu haiondoi uajabu wa mandhari ya kijiografia, kijamii na hata kiwakati. Kuhusiana na wakati, tungo zote tatu zinakiuka kabisa mpito halisi wa kiwakati. Hili linadhihirika katika kurejelewa kwa umri wa watu, muda ambao baadhi ya matukio yanachukua na tarehe ambapo matukio yanayohusika yalitokea. Kwa mfano, katika *Mafamba*,

tunaelezwa kwamba Amrao alifanya uhalifu wa kisiasa ambao unarejelewa kama “kumwaga mchanga ndani ya kitumbua”, akahukumiwa kifungo cha “miaka 30 mara tatu na tatu...” (uk.27) Mfano wa umri mkubwa ajabu wa Maotad umetajwa hapo juu. Katika kitabu hichohicho kuna mfano mwingine wa Damisi, ambaye tunaelezwa ni mzee wa miaka 777 (uk. 114) Kitabu tunachozungumzia pia kina mfano wa tarehe ya tukio muhimu la uchaguzi mkuu, uliofanyika 12/27/2200 nchini NUKA. Mtindo huu wa kuchezea vipimo vya wakati na kurejelea tarehe ambazo hazina uhalisi wa kihistoria unajitokeza katika tungo zote tatu. Katika *Mashetani wa Alepo*, tukio muhimu la mauaji ya kikabila nchini Alepo yaliyotekelvezwa na kundi la Megido lilitokea mwaka wa 3020 (uk. 10) Katika *Watu wa Gehenna*, tunaambowiwa kwamba machafuko yaliyosababishwa na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Kuhisika yalitokea mwaka wa 2047 (uk. 125).

Mbali na ukiukaji wa kaida za riwaya unahohusiana na uhusika na mandhari ya kiwakati, kijiografia na kijamii, pia kuna ukiushi mintarafu ya simulizi ambayo ni mfululizo wa visa vinavyohusiana. Mpangilio wa visa hivyo ndio unaounda msuko. Kama tujuavyo, msuko ni kijenzi muhimu cha riwaya ya kikaida. Chambilecho Boulton (1975: 45), “Msuko ni muhimu katika riwaya kama vile ambavyo kiunzi ni muhimu kwa mwili wa binadamu.” Anaendelea kuelezea kwamba msuko ndio unaoipa riwaya muundo na upatanifu. Msuko hutumia mbinu kama vile taharuki, analepsia, prolepsia na motisha zinazofanya kazi inayohusika ivutie. Tungo tatu za Olali ambazo tunazungumzia hazina msuko. Badala yake, zina mfululizo wa visa vinavyovunjikavunjika, na visivyo na uhusiano ulio wazi. Matendo ya wahusika ni ya kiajabu na hayana motisha. Kwa mfano, mwanzoni mwa *Mafamba*, tunamuona Arijoo akiikemea picha ya Maotad. Anapandwa na hasira na kupiga kelele: “Aende lazima ataenda. Maotad ni sharti aende.” (uk. 6) Sababu ya kitendo cha Arijoo haijitokezi wazi, yaani hakina motisha. Aidha, kitendo hicho hakina uhusiano ulio wazi na vitendo vyake vya baadaye. Mbali na ukiukaji wa kaida za riwaya katika tungo za Olali ambao umeshughulikiwa hapo juu, tungo hizo zina sifa nyingine za kifani ambazo, japo sio ukiushi wa moja kwa moja, zinazifanya kazi hizo kutofautiana sana na riwaya za kikaida. Kwanza, kuna suala la matumizi ya lugha, ambapo sifa zifuatazo zinajitokeza:

- a) Maelezo ya kinathari kukatizwakatizwa na matini za aina tofauti. Mfano wa matini ambazo zinakatiza mtiririko wa kinathari ni nyimbo. Katika *Mafamba*, tunapata nyimbo zifuatazo: (a) wimbo mrefu wa ukurasa mmoja na nusu ambao wafuasi wa Maotad wanatunga kuwajibu wapinzani – uk. 8-10 (b) wimbo wa karibu ukurasa mzima ambao Amrao anaimba akiwa kifungoni – uk. 27-28 (c) wimbo mrefu wa karibu kurasa mbili ambao Maotad anaimba kujibuu ule wa Amrao – uk.29-30 (d) wimbo mrefu wa karibu kurasa mbili ambao LiMioe anaimba – uk. 35-37 (e) wimbo mrefu wa Maotad – uk. 52-54. (f) wimbo wa karibu kurasa

mbili ambao paka wanamwimbia mtoto – uk. 92-94, n.k. Nyimbo fupi na ndefu pia zinajitokeza kwa wingi katika *Mashetani wa Alepo*. Katika *Watu wa Gehenna*, tunapata matini ndefu ya rejesta ya kisheria, ambayo ni mashtaka yanayowasilishwa dhidi ya Bi Saeeda Khan na Bi Rebecca Balira – uk. 82-101.

- b) Kiwango cha juu cha kuchanganya msimbo na kuhamisha msimbo. Mbali na maneno na sentensi nyingi za lugha za kigeni kama vile Kiingereza, Kiluo, Kilatini na Kigiriki, kuna vifungu virefu vya lugha za kigeni. Kwa mfano, (a) Samaki-binadamu anayesimulia juu ya maisha yake katika *Mashetani wa Alepo* anasema: “*I shall be methodological and cause maximum collateral damage. I will not spare anyone.*” “*I am not revengeful. Just doing a job. A clean job. Not a dirty job. I will come back in the strangest forms yet. In the form of a malady. A disease. An epidemic. It will begin from the airport. It shall be catastrophic. The human race must be wiped out.*” (uk.169-170)
- c) Wingi wa miundo ya sentensi inayokiuka kanuni za kisarufi, haswa sentensi zisizokamilika. Kwa mfano, katika *Mashetani wa Alepo* tunapata mifano ifuatayo: (a) Nyumbani kwa Nabhany. Matondoni. Watu walivyoishi. Utamaduni mtamu – uk. 111 (b) Aliusukuma. Wapi. Tena. Wapi – uk. 140

Maelezo ya hapo juu yanatosha kudhihirisha jinsi tungo tunazoshughulikia zilivyo tofauti na riwaya za kikaida. Turejelee lile suala la uainishaji wa tungo hizo. Ni wazi kwamba tungo za Olali ni zao la umajaribio. Istilahi hii inamaanisha uumbaji wa sanaa kwa kuzua kunga na mitindo mipyä ambayo inakiuka kimakusudi kaida zilizozoleka. Wasanii hufanya hivyo kama uasi dhidi ya kaida za uandishi ambazo wanazona kama kizingiti cha ubunifu na uzalishaji wa sanaa mpyä. Mtazamo kama huu ndio uliozaa matapo k.v. Usasa na Usasaleo, riwaya mpyä na Ushairi huru. Kwa hiyo, kazi tunazozungumzia ni aina ya binilizi ya kimajaribio ambayo inaweza kurejelewa kama dhidiriwaya. Tungo za aina hii huvunja kimakusudi kaida za uandishi wa riwaya zilizotajwa hapo juu. Katika fasihî ya Kiswahili, tungo za aina hiyo zilianza kujitokeza katika miaka ya 1990 ambapo mwandishi wa Tanzania, Euphrase Kezilahabi, aliandika *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991). Kazi za Olali ni mwendelezo wa jadi hiyo ambayo ni mwigo wa matapo ya Ulaya ya Usasa na Usasaleo.

Kwa jumla, maudhui ambayo dhidiriwaya tatu za Tom Olali zinashughulikia yanagonga ndipo kwa msomaji wa Afrika Mashariki. Hivi ni kwa sababu yanahusiana na changamoto ambazo wananchi wa kanda hii wanakabiliana nazo katika maisha yao ya kila siku. Isitoshe, maudhui hayo yanaweza kutoa mchango katika kuimarisha mshikamano wa kitaifa kama yangeifikia hadhira inayohusika. Kwa mfano, *Mafamba* inashughulikia usaliti wa kisiasa ambao Wakenya

walifanyiwa na viongozi wao katika kipindi cha tangu ukombozi wa pili na kuundwa kwa serikali ya NARC (National Rainbow Coalition) mwaka wa 2002. Katika siasa za Kenya, “ukombozi wa pili” unarejelea harakati za kisiasa ambazo zililenga kukiiondoa madarakani chama tawala cha KANU (Kenya African National Union) katika miaka ya 1990. Kilele cha harakati hizo kilikuwa kuundwa kwa NARC ambao ulikuwa muungano wa vyama kadha nya upinzani mwaka wa 2002. Huo ulikuwa mwaka wa uchaguzi mkuu ambao matokeo yake yalikuwa kushindwa kwa KANU kwa mara ya kwanza tangu uhuru mwaka wa 1963. Hili lilikuwa tukio la kihistoria ambalo lilibadilisha siasa za Kenya. Usaliti unaohusika ni kwamba serikali mpya iliyoongozwa na Mwai Kibaki ilitoa ahadi chungu nzima za kujenga upya taifa ambalo lilikuwa limedhoofishwa na utawala mbaya wa KANU. Lakini utawala mpya uliyumbishwa na ujisadi, ukabila na maovu mengine, ukashindwa kutimiza ahadi zake.

Hitimisho

Kwa kiwango kikubwa, kazi tunayozungumzia inatumia mtindo wa istiara, ambapo wahusika, matukio na mandhari yanahusiana moja kwa moja na watu, matukio ya kisiasa na mahali halisi nchini Kenya katika kipindi kilichotajwa hapo juu. Kwa mfano, bara la Afrika linarejelewa kama Karifa; nchi inarejelewa kama sayari. Jiji la Nairobi limepeewa jina la ajabu la Bikerani-Msiige. Kenya chini ya utawala wa KANU inarejelewa kama NUKA; Kenya chini ya utawala wa NARC ni BORA. Majina halisi ya watu walioshiriki katika matukio halisi ya kisiasa yamepinduliwa kwa njia mbalimbali, lakini baadhi yanafasirika. Nayo ni kama yafuatayo: Maotad – Daniel Arap Moi; LiMioe (kutokana na jina lake lisilo rasmi, Emilio) – Mwai Kibaki; Amrao – Raila Amolo Odinga; Shanata – Sharif Nassir Tayib; Rojoo – Robert John Ouko; Sinya – Simeon Nyachae; Fadhila (kutokana na tafsiri ya jina lake la kwanza) – Charity Ngilu; Boyi – Michael Kijana Wamalwa; Saigeo – George Saitoti; Kajo – Joseph Kamotho; Kanga – Katana Ngala; Kamu – Kalonzo Musyoka; Nikiabi – Kipyator Nicholas Biwott; Jogi – John Githingo, n.k. ilivyo ni kuwa vidokezo ambavyo tumetoa hapo juu vinatosha kutuwezesha kuyafikia mahitimisho muhimu juu ya tungo zinazohusika mintarafu ya mada tunayoshughulikia. Ni wazi kwamba *Mafamba, Watu wa Gehenna na Mashetani wa Alepo* zinachunguza hali halisi ya siasa za Afrika Mashariki na Afrika kwa jumla, na kuangazia athari za hali hizo kwa maisha ya walio wengi. Mbali na maudhui ya kisiasa, kuna mengine chungu nzima ambayo yanagusiwiguswa. Kwa kweli udhaifu mmoja wa kazi hizo, haswa *Watu wa Gehenna*, ni kugusiwiguswa kwa mambo mengi sana ambayo hayashughulikiwi kwa kina kama inavyostahiki. Pamoja na hayo, maudhui hayo yanafaa kwa hadhira ya Afrika Mashariki. Ni wazi kwamba hii ndiyo hadhira ambayo mwandishi alilenga. Maudhui hayo ya kupinga maovu ya kisiasa na mengineyo yanachangia katika kukuza thamani za kitaifa ambazo ni muhimu katika kujenga mshikamano wa kitaifa. Huu ni upande chanya wa tungo za kimajaribio

zinazohusika. Upande hasi wa kazi hizo unahusiana na umajaribio wake. Kwanza ni muhimu kuweka wazi kwamba hatupingi umajaribio katika fasihi. Hivi ni kwa sababu unazalisha mitindo mipya na hatimaye fasihi mpya. Lakini kuna suala la umajaribio unaofaa katika mazingira yetu. Kuhusu suala hili, tunaunga mkono msimamo wa Chinweizu na wengine. Wanasisitiza kwamba umajaribio unaofaa katika fasihi ya Kiafrika sio ule unaofuata mkondo wa Usasa wa Kimaghari, bali ule unaofufua na kuendeleza jadi simulizi ya Kiafrika. Wanaendelea kusema: "Msanii katika utamaduni wa kijadi wa Kiafrika aliongelesha jumuiya na aliongea kwa niaba ya jumuiya. Jazanda zake, dhamira, taashira na fani kwa jumla zilichotwa katika dimbwi la pamoja la jumuiya nzima." (TY) Hivi ni kusema kwamba mwandishi anawajibika kuwasilisha maudhui yake kwa kutumia fani ambayo itayawezesha kuifikia hadhira yake. Tatizo la tungo za Olali ni kwamba kutokana na mkondo wa umajaribio anaofuata, zinaishia kuwa na fani ambayo ni ngumu sana kwa msomaji wa kawaida kuweza kuifasiri. Hii inayafanya maudhui yake mazito na yanayostahili kusambazwa yasiweze kuifikia hadhira iliyolengwa. Kuna hatari ya kazi kama hizo kuishia kuwa data tu ya wanazuoni badala ya sanaa inayochangamkiwa na wasomaji walio wengi. Kwa sababu hizo, tungo za Olali zinatoa mchango hafifu katika kuleta mshikamano wa kitaifa.

Marejeleo

- Baldick, C. (2001). *Oxford Dictionary of Literary Terms*. New York: Oxford University Press.
- Boulton, M. (1975). *The Anatomy of the Novel*. London: Routledge & Kegan Paul.
- Chinweizu, na wenzake, (1983). *Toward the Decolonization of African Literature*. Enugu: Fourth Dimension Publishing.
- Dorsch, T. S. [mfas.] (1965). *Classical Literary Criticism*. New York: Penguin Books.
- Fanon, F. (1967). *Black Skin White Masks*. New York: Grove Press.
- Fischer, E. (1959). *The Necessity of Art*. London: Penguin Books.
- Kezilahabi, E. (1979). *Gamba la Nyoka*. Arusha: Eastern African Publishers.
- Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Kezilahabi, E. (1991). *Mzingile*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mlacha, S. A. K. na Madumulla, J. S. (1991). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Nazareth, P. (1978). *The Third World Writer: His Social Responsibility*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Okoth, A. (2006). *A History of Africa Vol.1*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Olali, T. (2008). *Mafamba*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Olali, T. (2012). *Watu wa Gehenna*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Olali, T. (2015). *Mashetani wa Alepo*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

- Vazquez, A. S. (1973). *Art and Society*. London: Merlin Press.
- Wa Thiong'o, N. (1972). *Homecoming*. London: Heineman.
- Wa Thiong'o, N. (1981a). *Writers in Politics*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Wa Thiong'o, N. (1981b). *Decolonizing the Mind*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Wanjala, C. (1978). *The Season of Harvest*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Wellek, R. na Warren, A. (1949). *Theory of Literature*. New York: Penguin Books.

